Mkakati wa Taifa wa kudhibiti
UKIMWI (2008 – 2012) kwa ufupi

Lugha rahisi ya mkakati wa Taifa wa kudhibiti Ukimwi (2008 – 2012), Kwa Mashirika madogo madogo ya kijamii (CSO's)

Imetayarishwa na:
Tanzania Aids Forum
P.O.BOX 65147
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 55 09422
Fax:+255 22 2772299
Barua pepe: info@tzaidsforum.org
Tovuti: www.tzaidsforum.org

1.0. Kwanini lugha rahisi imetengenezwa?

Lugha rahisi imetengenezwa ili kuwezesha mkakati kueleweka kwa kila mdau wa mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI Tanzania, pia kufanya utekelezaji wa mpango pamoja na rasimu ya Ukimwi kuwa rahisi kuanzia ngazi ya mtu binafsi, familia, jamii, asasi zisizokuwa za kiserikali (Azaki) mpaka taifa kwa ujumla wake.

2.0. Kwanini Tanzania iliandaa na kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI?

Tanzania iliandaa na inaendelea kuutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI kutokana na ukweli kwamba janga la UKIMWI ni tishio kubwa kwa mikakati ya maendeleo inayofanywa na sekta zote na wakati mwingine linaathiri maendeleo yaliyofikiwa awali. Athari za janga hili zinasababisha machungu kwa mtu mmojammoja, familia na hata jamii yote nchini. Hata hivyo, kuna dalili za matumaini, kwa mujibu wa taarifa za hivi karibuni kiwango cha maambukizi ya VVU kinapungua kwa kiasi kikubwa katika maeneo mengi nchini.

Kwahiyo, hivi sasa Tanzania inatekeleza Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2008-2012. Inaimarisha mafanikio yaliyofikiwa katika mwitikio wa Taifa kwa janga la UKIMWI (2008 – 2012) katika miaka mitano iliyopita (2003-2007) na kupendekeza hatua na mikakati ya kupambana na vikwazo na changamoto zilizojitokeza katika kipindi hicho. Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI unatoa mwongozo wa mbinu za kupambana na janga hili pamoja na shughuli ambazo zitatekelezwa na wadau wote nchini ikiwa ni juhudi za kuwa na mkakati mmoja unaowaunganisha wadau na sekta zote.

TANZANIA AIDS FORUM

3.0. Tunatarajia mafanikio gani kutokana na Mkakati huu?

Tanzania ina dira na dhamira ambayo tungependa kuifanikisha katika miaka mitano ijayo ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI 2008-2012.

Dira: "Tanzania inaendeleza juhudi za pamoja za kupunguza kuenea kwa VVU na kutoa matunzo bora

Dhamira: Kutoa mwongozo wa kulinda uongezaji na upanuzi wa ubora wa kinga, matunzo na msaada dhidi ya VVU/UKIMWI na kuwa na ushawishi mkubwa kwenye programu na shughuli mbalimbali za kudhibiti na kupunguza athari ndani ya programu ya mwitikio shirikishi wa Taifa yenye uratibu mzuri unaoongozwa na Serikali Kuu, kushikizwa kwenye Halmashauri za Serikali za Mitaa, kujikita ndani ya jamii na kusaidiwa na wadau wote wanaohusika.

3.1. Ni kwa jinsi gani tutafanikisha kufikiwa kwa dira na dhamira hii?

Ili kufanikisha kufikiwa kwa dira na dhamira, Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI 2008-2012 unasisitiza malengo manane yanayohitaji kufikiwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo nayo ni kama yafuatayo

1. *Kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha washirika wote kushiriki kikamilifu katika mwitikio wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI*
2. *Kupunguza kiwango cha maambukizi ya VVU nchini.*
3. *Kupunguza maradhi na vifo vitokanavyo na VVU/UKIMWI.*
4. *Kuboresha kiwango cha maisha ya watu wanaoishi na VVU na wale walioathiriwa na VVU wakiwamo yatima na watoto wengine wanaoishi katika mazingira hatarishi.*
5. *Kutumia ushahidi unaofaa na wa kutosha uliotolewa kwa wakati katika mipango inayohusu VVU na utoaji maamuzi.*
6. *Kusisitizia uwazi, uwajibikaji wa viongozi na vyombo vyote vinavyojishighulisha na udhibiti wa VVU na UKIMWI*
7. *Kuhakikisha pesa, vifaa na wataalamu wanapatikana kwa ajili ya utekelezaji wa mwitikio hususan kwenye hospitali na zahanati na kliniki*
8. *Kuhakikisha mkakati wa Taifa unawekewa mipango mizuri ya utekelezaji katika ngazi zote kuanzia Katika Taifa hadi vijijini.*

3.2. Je kuna kitu kitakachofanyika tofauti na Mkakati wa siku za nyuma?

Ndio, kuna tofauti kwa kiasi fulani, japo yaliyofanywa na mkakati uliopita hayataachwa kwani yanajenga na kukamilishwa katika mkakati huu. Mkakati huu umetoa kipaumbele katika mambo matatu yafuatayo:

1. Kuongeza juhudi za kinga dhidi ya VVU
2. Kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata huduma bora na endelevu za VVU na Ukimwi.
3. Uchunguzi wa vipaumbele vya ufua katika maeneo yaliyodhamiriwa ya mazingira yanayowezesha, kinga, matunzo na matibabu pamoja na upunguzaji wa athari lazima uzingatie hali halisi ya mahali wakati wa kufasiri Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI katika mipango ya utekelezaji



4.0. Mikakati katika maeneo muhimu manne

4.1. Eneo la 1: Mazingira yanayowezesha Malengo kufikiwa.

Mazingira yanayowezesha kuwa na mikakati thabiti inayoendana na maeneo husika na mahitaji kwa kipindi hicho, hususani kwa kuangalia visababishivya ongezeko la maambukizi na ukosekanaji wa huduma bora na matibabu.

Matokeo muhimu kwenye eneo hili

- *Kuhimiza uwazi na uwajibikaji katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na utungwaji wa sheria na kupata viongozi bora*
- *Kuhakikisha haki za binadamu na usawa wa kijinsia vinahushishwa katika shughuli za utetezi na uraghbishi mfano unyanyapaa, kujikataa na ubaguzi katika ngazi zote za jamii*

- *Kushirikisha vikundi mbalimbali vya watu waishio na VVU katika shughuli za uraghbishi*
- *Kuhakikisha ubora wa upatikanaji wa taarifa za namna ya kujikinga na maambukizi, matunzo,tiba pamoja na huduma za kupungaza athari za UKIMWI kwa wanaoishi na VVU*
- *Kuweka mazingira endelevu ya kisiasa, kijamii na kiutamaduni ambapo masuala ya ngono na ujinsia yanaweza kujadiliwa kwa uwazi.*
- *Kuhimiza, kuwezesha na kupanua mifano ya uhamasishaji jamii kuhusu VVU katika Wilaya zote*
- *Kuimarisha ushiriki wa asasi za kiraia, uongozi wa kisiasa na uongozi wa kijamii katika kufanya utetezi na uhamasishaji wa jamii katika kuanzisha na kutekeleza afua za jamii*
- *Kuhimiza matumizi ya mfumo wa ufuatiliaji wa TOMSHA*
- *Kufuatilia na kutathmini mipango ya uhusishaji wa VVU/UKIMWI ili kuboresha utendaji na kutoa taarifa muhimu zitakazosaidia usimamizi mzuri wa programu*

Je ni maswali gani ya kutumia kutathimini eneo hili?

- Je kuna uwazi na uwajibikaji kuhusu UKIMWI katika jamii yako/yetu ?
- Je haki za binadamu na usawa wa kijinsia kuhusu UKIMWI vinazingatiwa katika jamii yako/yenu ?
- Je taarifa sahihi za kujikinga na UKIMWI na matunzo zinapatikana katika jamii yenu ?
- Je Asasi za Kiraia zinashirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wa TOMSHA ?

TANZANIA AIDS FORUM

Eneo la 2. ***Matunzo, Matibabu na Misaada***

Mikakati kadhaa imebainishwa hapa chini kuteleleza na kufikia malengo hayo. Ni muhimu sana kunoa huduma zinawafikia walengwa na zenye ubora unaohitajika.



- Kuongeza uwezo wa kupanga, kutekeleza, kuratibu, kufuatilia na kutathmini ubora na uhakika wa huduma za matunzo, matibabu na misaada ambazo ni endelevu.
- Kuongeza idadi ya watoa huduma wenye utaalamu

- Kupanua wigo wa upatikanaji na uwezekano wa kufikika kwa huduma za dawa na tiba za magonjwa nyemelezi

- Kujenga ushirikiano na waganga wa tiba za jadi katika utoaji endelevu wa matunzo, matibabu na misaada

- Kuimarisha uhusiano baina ya huduma endelevu za matunzo, matibabu, misaada na huduma nyingine pamoja na huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, ushauri nasaha na upimaji wa VVU, udhibiti wa magonjwa ya ngono na kuhakikisha upatikanaji na matumizi sahihi ya kondomu

- Kuimarisha utoaji wa elimu na taarifa zitakazofanikisha mabadiliko ya tabia katika nyanja za matunzo, matibabu na misaada kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI, inayowalenga watoa huduma na watu wanaotarajiwa kunufaika na huduma hizo

- Kuingiza suala la ushauri nasaha kuhusu lishe, elimu na misaada katika matunzo na matibabu kwa watu wanaoishi na VVU na watoa huduma, ikiwa ni pamoja na kubadilisha mlo kulingana na aina za vyakula vinavyopatikana katika eneo husika

- Kuhimiza ushiriki mkubwa wa watu wanaoishi na VVU katika kupanga na kutekeleza programu za huduma majumbani na misaada

- Kuhakikisha kwamba watoa huduma wanafahamu haki na stahiki ya matunzo, matibabu na misaada kwa mujibu wa Miongozo ya Taifa ya Utoaji wa Huduma za Majumbani

- Kuhimiza uraghibishi na elimu kwa umma katika jamii ili ziweze kukidhi ipasavyo mahitaji ya watu wanaoishi na VVU na familia zao

- Kuimarisha uhusiano wa kiutendaji zikiwemo huduma za rufaa kati ya vituo vya huduma za afya na huduma za majumbani

4.2. Eneo la 3: Kupunguza Athari zitokanazo na UKIMWI

Kuna mikakati mingi mizuri inayolenga katika kupunguza athari zitokanazo na UKIMWI. Jambo la muhimu ni kuhakikisha kuwa mikakati inalenga mazingira husika na inaleta tija na kufanikisha kuyafikia malengo. Mikakati yenyewe tunayoweza tumia ni kama ilivyoainishwa hapa chini.

- Kuimarisha uwezo wa familia, majirani na jamii katika kuwalinda na kuwatunza watoto walio katika mazingira hatarishi zaidi

- Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora na za muhimu kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wanaohitaji sana msaada

TANZANIA AIDS FORUM

- Kutambua matatizo makubwa yanayozipata kaya zinazoongozwa na watoto na wazee wenye watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi
- Kujenga mazingira mazuri kwa watoto wote walioathiriwa na VVU na UKIMWI kupitia utetezi na uhamasishaji wa jamii
- Kuimarisha uwezo wa taasisi muhimu katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya na ngazi ya jamii ambao ndio wanaowajibika kuratibu mwitikio wa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, kuhusisha miitikio ya taasisi katika mifumo iliyowekwa na Serikali
- Kufuatilia na kutathmini miitikio ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi nchini Tanzania, kwa kuweka mkazo katika namna ambavyo huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi zinavyosaidia katika kupata matokeo mazuri katika kaya, familia, ndugu na jamaa, majirani na jamii kwa ujumla
- Kuwaangalia zaidi watu wanaotoa matunzo wenye mahitaji maalumu, ikiwa ni pamoja na wazee, watoto, watoa huduma walio katika hali mbaya kiafya, na watoa huduma wenye ulemavu, na kutambua tofauti ya majukumu baina ya wanawake na wanaume
- Kuimarisha mitandao ya wahudumu wa jamii wanaojitolea, na mitandao ya misaada ya kijinsia katika rika, kutambua na kuwajibika kwa kuwa wanawake na wanaume ni wadau
- Kupunguza unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya kaya zinazowatunza watu wenye VVU, kupitia majadiliano na kazi za kijamii, utambuzi wa hali tofauti na athari zinazowakabili wanawake na wanaume
- Kupanua kazi za kijamii zinazozingatia haki, utambuzi wa athari tofauti kwa wanawake na wanaume
- Kuviwezesha vikundi vya kijamii vilivyo rasmi na visivyo rasmi kuweza kupanua shughuli za kusaidia makundi yaliyoko hatarini zaidi
- Kutafuta njia za kupanua fidia za bima kwa wale wenye VVU katika sekta rasmi.

Je ni maswali gani ya kutathimini eneo hili?

- Je jamii infahamu wajibu wao katika kuwatunza na kuwalinda watoto walio katika mazingira hatarishi zaidi?

- Je watoto waishio katika mazingira magumu na hatarishi wanapata wanapta huduma muhimu na bora zinazostahili ?

- Je jamii ina elimu ya kutosha kuhusu unyanyapaa na athari zake kwa watu waishio na VVU?

- Je Asasi za Kiraia zinajengewa uwezo katika kuratibu mwitikio wa jamii kuhusu watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kuhusisha miitikio ya taasisi katika mifumo iliyowekwa na Serikali?

4.4. Eneo la 4: Kuzuia Maambukizi

Inaonekana hali halisi ya maambukizi kupungua kwa kiasi kitaifa, lakini kuna baadhi ya maeneo maambukizi yameongezeka na tabia hatarishi zinaendelea. Mikakati kadhaa imependekezwa ili kusaidia kupunguza au kuzuia maambukizi. Mikakati ya kuzuia maambukizi iliyopendekezwa, itafaa kutumika kutokana na hali halisi ya vihatarishi katika eneo husika. Baadhi ya mikakati iliyopendekezwa ni kama ifuatavyo:

1. Kuwajengea uwezo wazazi na walezi ili waweze kuzungumza na watoto kuhusu masuala ya UKIMWI, kujamiiana na afya ya uzazi.
2. Kutoa changamoto kwa mila na desturi na mfumo unaosababisha wanawake kuwa dhaifu kwenye familia, shuleni na katika jamii
3. Kukuza na kuendeleza elimu rika na kutoa mafunzo kwa washauri nasaha kwa vijana walioko shuleni na nje ya shule
4. Kuongeza utoaji wa huduma tarifa za afya ya uzazi kwa kuziunganisha na shughuli za maisha na shughuli za kuongeza kipato
5. Kutangaza na kupanua programu dhidi ya dawa za kulevya hasa unywaji wa pombe uliokithiri.
6. Kwa kuwatumia wanaume mashuhuri, kuwashawishi na kutangaza usawa wa kijinsia.
7. Kupitia na kuboresha sheria zinazopuuza ndoa za utotoni a wasichana (kabla ya miaka 18)
8. Kujenga ubia kati ya Serikali na asasi za kijamii pamoja na taasisi
9. Kupanua wigo na ubora wa huduma za magonjwa ya ngono, taarifa za kinga, na huduma ya waviu
10. Kupanua ushauri nasaha na upimaji wa hiari unaokubalika kijamii, rafiki kwa vijana na unaozingatia jinsia katika vituo vya huduma za afya na vile vinavyojitegemea

11. Kushawishi na kuhamasisha jamii katika ngazi zote kuhusiana na kudhibiti maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na kushughulikia masuala ya unyanyapaa

12. Kuunganisha wanawake walioathirika na VVU pamoja na watoto wao katika vituo vya huduma, matibabu na matunzo

13. Kupanua uwepo na upatikanaji wa kondomu bora katika maeneo yote nchini kupitia mikusanyiko ya kijamii na kuimarisha na kubadilisha mbinu za ugawaji bure wa kondomu kwa umma

14. Kushawishi viongozi wa dini wanaopinga matumizi ya kondomu ili wakubaliane na matumizi hayo hasa kwa wapenzi ambao mmoja wao ameathirika

15. Kutoa habari kwa jamii nzima zinazohusu hatari ya maambukizi ya VVU kwa kupitia shughuli za kimila zinazochangia maambukizi na kuwahusisha watendaji katika upunguzaji hatari ya maambukizi

16. Kuhamasisha na kueneza njia bora za kutahiri wanaume kama njia ya kuzuia maambukizi mapya wakati huohuo kuchukua tahadhari ya madhara yanayoweza kutokea

5.0 Mfumo na Mpangilio wa utelelezaji wa mwitikio wa Taifa.

Lengo ni kutoa mpango ulioratibiwa vizuri, unaofaa, wa uwazi, unaowajika na wakudumu, pia muundo wa menejimenti kwa kuzingatia 'kanuni ya dhana tatu' katika ngazi ya Taifa, Mkoa na mamlaka za serilkali za mitaa ili kutoa mwitikio unaohusisha wadau kutoka sekta za umma, binafsi na vyama vya kiraia.

Mfumo wa kitaasisi na menejiment hutoa mwelekeo wa jinsi mwitikio wa kitaifa utakavyopangiliwa na kuratibiwa.
Ili kurahisisha utekelezaji, ufuatiliaji na uwajibikaji wa mwitikio wa Ukimwi mkakati umeanisha ngazi zote (kitaifa, mkoa wilaya mpaka ngazi ya serikali za mitaa). Katika ngazi ya kisiasa, vyama vya siasa, bunge, baraza la mawaziri na ofisi ya waziri mkuu ndio vyombo vikuu vya usimamizi, wakati Tume (TACAIDS) ndio wanaoratibu.

- Vyama vya siasa
- Bunge
- OWM-TAMISEMI
- Wizara,Idara na Wakala za serikali
- Tume ya kudhibiti ukimwi (TACAIDS)
- Tanzania National Coordinating Mechanism (TNCM)

Vyama vya siasa

Vyama vya siasa ni muhimu katika kuweka agenda za Ukimwi kwenye vikao vyao, pamoja na kusimamia, vilevile hutoa ushauri kwa serikali ili utekelezaji wake uwe shirikishi.

Bunge

Chombo hiki kinawajibika katika mwitikio wa Ukimwi kupitia taarifa kutoka wizara mbalimbali na tume ya taifa ya ukimwi. Kupitia kamati ya Ukimwi ya bunge (TAPAC), bunge linatoa ushauri kwa wizara na serikali za mitaa kwa lengo la kuboresha utekelezaji na kuongeza mapambano.

OWM-TAMISEMI

Tawala za mikoa na serikali za mitaa in chombo muhimu katika utekelezaji ndani ya mfumo wa kupunguza majumu ya serilaki kuu kwa kupeleka madaraka mikoani. Tamisemi inaratibu shughuli za mamlaka za serikali za mitaa pia inasimamia na kusaidia program zake.

Wizara,Idara na Wakala za serikali

Vyombo hivi vinatakiwa kuimarisha na kupanua shughuli zao za Ukimwi, kwa kuunda, kutekeleza na kusimamia miradi ya Ukimwi katika sehemu za kazi kwa wafanyakazi na familia zao.

Tume ya kudhibiti ukimwi (TACAIDS)

Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi ndio waliopewa dhamana ya kuongoza, kupanga na kuratibu utekelezaji wa mwitikio wa Ukimwi kitaifa kupitia ofisi ya waziri mkuu. TACAIDS inamajukumu yafuatayo:-

- Kutoa ushauri na kusaidia serikali za mikoa, wilaya na mitaa kupitia wizara ya tawala za mikoa na serikali za mitaa (TAMISEMI), Azaki (FBO’s. NGO’s, CBO’s n.k).

Tume ya Taifa ya Ukimwi inawajiika kwa Katibu mkuu ofisi ya Waziri mkuu.

AZAKI

Asasi zisizokuwa za kiserikali zitaendelea kuchangia kufanikisha mwitikio wa Ukimwi katika jamii. Kwa upande mwingine AZAKI zinafanya kazi Kwa niaba ya serikali ya kutoa huduma ya UKIMWI katika jamii na familia, ikiwa ni pamoja na kuangalia je serikali inafanya kile ambacho inapaswa kukifanya kwa jamii kulingana na vipaumbele vilivyowekwa kwa manufaa ya jamii?

Utaratibu wa uratibu wa kitaifa - Tanzania (TNCM)

Mtandandaomuhimu ambao unasimamia na kuratibu matumizi ya fedha za mfuko wa dunia (Global fund) inchini. Chomo hiki kina wawakilishi kutoka sekta zote Serikali, Azaki, Mashirika binafsi n.k. Chombo hicho husimamia matumizi ya pesa hizi katika kukabiliana na Ukimwi, Maralia. TB na masuala mengine ya afya, katika utaratibu uliopangwa na kushirikisha kila sekta nchini.

Muundo wa Raslimali fedha, Watu na Vitendea kazi kwenye mwitikio wa Kitaifa

Lengo ni kutoa raslimali muhimu zinazofaa za kifedha na vitendea kazi kwa ajili ya utekelezaji wa mwitikio wa kitaifa wa kupambana na VVU kwa kupitia juhudi shirikishi, zilizoratibiwa na endelevu za serikali ya Tanzania, sekta binafsi na za kijamii na wabia wa maendeleo.
Muundo wa raslimali za mkakati huu kwa mwaka 2008 – 2012 umeanisha maeneo muhimu matatu ambayo ni raslimali fedha, watu na vitendea kazi.

Raslimali fedha

Katika mwitikio wa kitaifa, Tanzania inategemea ufadhili kutoka kwa serikali ya marekani, mfuko wa kitaifa wa kupambana na ukimwi, kifua kikuu na Malaria (GFATM) na Benki ya dunia kwa aslilimia 80%.
Wizara pamoja na serikali za mikoa na wilaya zinapata fedha kutoka serikali kuu kupitia mkakati wa muda mrefu kuhusu VVU na Ukimwi kwenye mipango ya matumizi ya muda wa kati (MTEF). Vilevile halmashauri za wilaya hupata pesa za kupambana na maambukizi kutoka TASAF RFE etc, Wakati mashirika yasiyo ya kiserikali hutegemea zaidi wafadhili katika utekelezaji wa mwitikio wa kitaifa wa VVU na Ukimwi. Mkakati unaeleza mwongozo wa mtiririko wa fedha katika nchi kutoka kwa wadau kwenda kwa wapokeaji. Taratibu hizi zinajumuisha kusaidia bajeti kuu (GBS), Mfuko wa fedha wa pamoja na utoaji wa moja kwa moja kwa taasisi husika.

Watumishi

Kama ilivyo ada watumishi ni nyezo muhimu katika utekelezaji wa mwitikio wa ukimwi wa kitaifa. Tanzania bado inapata changamoto ya watumishi wa kutosha hasa kwenye sekta ya afya wanaotekeleza mwitikio wa VVU na Ukimwi. Mfano kwa miaka mitano iliyopita sekta ya umma ambayo ndiyo yenye wafanyakazi wengi imeshuhudia kupungua kwa idadi kubwa ya wafanyazi wa afya licha ya kuongezaka kwa mahitaji ya huduma ya matunzo na msaada kwa watu waishio na VVU.

Vitendea kazi

Katika utekelezaji wa mwitikio wa ukimwi wa kitaifa, kuna vitendea kazi vingi katika utaratibu mzima wa kupambana na VVU; usambazaji wa bidhaa kama Kondomu, ARV na vifaa vya maabara kwa mlolongo wa shughuli kama vile kufanya mikutano n.k. tatizo ni katika usimamizi muundo wa ugavi, manunuzi na matatizo ya usafirishaji.

TANZANIA AIDS FORUM